# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

KIDATO CHA NNE

MTIHANI WA PAMOJA WA MOMALICHE 3

MSURURU WA NANE

MWISHO WA MUHULA WA KWANZA

MWAKA 2021

MUDA SAA: 2 DAKIKA: 30

MAAGIZO

Jibu maswali yote kwenye karatasi hii.

1. UFAHAMU

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Macho makali ya Vuai yalipigwa na mwali mkai wa jua la asubuhi.Ilikuwa ndiyo mara ya kwanza kuuona mwanga halisi wa ombwe lijiitalo dunia tangu alipohukumiwa kifungo gerezani.Punde tu komeo la mlango wa seli lilipofunguliwa,ilimlazimu Vuai ayafumbe macho kabla ya kuyafumbua tena ili yazoee mabadiliko yake.

Ilikuwa ndiyo siku ya Vuai kuachiliwa huru kutoka kwenye kifungo kirefu kilichoyapa macho yake mazoea ya gizaa la kaburi mle gerezani.Macho yake yalipoookwishaizoea ile hali na kumhakikishia kuwa kila alichokuwa akkikioona si kizuka ila uhalisia,alipiga hatua.Akatoka nje ya mlango wa seli kisha kwa kutoamini,akageeuka nyuma kulitazama tena lile pango alimokuwa ametikwa katika muda huo wote.Akayafikicha macho kwa kutoamini huku machozi yakimdondoka asijue kama yalikuwa ya furaha au ya huzuni.Alipogeuka kuanza safari ya uhuru wake,macho yake yalikumbana na lengo la gereza.Hapo ,akasita kidogo,labda kuhakikisha kama kweli alikuwa huru.Bila shaka,hakuna askari wa gerez aliyemshikia bunduki au kumhanikizia sauti

asimame.Walimtazama tu na kumpa tabasamu.

Taratibbu,Vuai aliendelea kupiga hatua.Mhemko aliokuwa nao kutokanana hea safi iliyompenya mapafuni uliufaanya moyo wake upige kwa kasi.Ghafla ,tabasamu likapasua mashavuni pake.Akasita.Akainua pua yake iliyompa hakikisho kuwa fondogoo na uvundo wa esli haukuw naye tena.Ingawa  mwili wake ulijaa mabaka ya uchafu na matambara yaliyouficcha ucchi wake kuvunda,hilo halikumkera tena.Kwa hivyo,akatia teena tabasamu .Lake kuu lilikuwa ni shukrani kw kuepuka yale madhila ya joto na rundo la wafungwa.Na kama hilo halikutosha,aligeuka tena ili sasa kuliangalia lile gereza.Bila kutaraji,alipiga magoti,akainua mikono kupigs dua,"Ewe Munggu,niepushe na balaa nyingine".

Safari ya Vuai kutoka katika majengo ya gereza ilikumbwa na mset wa mawazo.Alipokuwa katika ujia uliomwelekeza katika barabara kuu,mambo mengi yalimpitikia mawazoni asipate jawabu.Hakujua kamawazazi wake wangali hai na kama bado walikuwa wanaishi katika nyumba ile ya kukodi kwa miaka hiyo kumi aliyokuwa jela"Je,nikiwakosa nitaenda wapi?Nitaanza wapi kuwatafuta ?"Mawazo haya yalifunguanmifereji ya machozi,kasha ile ya makamasi.Balagha hiyo iiyomfikisha katika kituo cha magari ya uchukuzi kwa ule aliouona kuwa muda wa kufumba na kufumbua.Aliyafuta machozi yake haraka kwa kiganja kasha akaziba tundu la pua,tayari kupenga kamasi.Hata hivyo,kabla hajafanya hivy,nafsi yake ilimtahadharisha kuwa hatua hiyo ingekatiza uhuru aliopewa kwa kuchafua mazingira.Kwa hivyo akaghairi .Akavuta ncha ya shati lake na kuitumia kama hankachifu kutimiza azma yake.

Hapo kituoni,matatu iliyokuwa mbele ilikuwa wa watu wachache.Vuai akaingia na kukaaa upande wa kioo ambapo tafakuri nyingi zilimjia.Akakumbuka jinsi kesi yake yake ilivyoendeshwa kinyume kabisa na ukweli na hukumu kutoelewa kinyume cha haki."Mimi Vuai,motto taa tangu kuzaliwa kwangu hata mdudu sijawahi kumponda kwa udole wangu,ndi sasa nije kusingiziwa kumpoka mtu  uzima?Mungu wangu!Kwa nini dunia hii haina wema?Kwa nini wanaodaiwa kuwa wasomi hata wakapewa jukumu lakuwakilisha maslahi ya raia ndi wanaowadhulumu hao raia?Hivi,hata hakimu na tajriba yake aliamua kufuatilia zile poroj za wanaojiita majasusi?Angeahirisha hukkumu yake ili kufanya uchunguzi zaid,bila shaka nisingepata mapig na dhuluma hizo zote.Kwa kweli hii ni dunia ya mwenye nguvu mpishe1"Vuai alijisemea.

a. Kwa nini Vuai alifungwa jela?

   *Alisingiziwa kumuua mtu*

b. Kwa kurejelea kifungu ,eleza madhila yaliyomo kwenye asasi za kurekebishia tabia

i. *Wafugwa hudhulumiwa*

ii. *Mazingira yenye uvundo/hewa si safi*

iii. *Watu hawaogi*

iv. *Kwa giza*

v. *Jua kali*

vi. *Msongamano*

c. Onyesha kinaya kinachojitokeza kwenye kifungu hiki

*Wasomi ambao wamepewa majukumu ya kuwakilisha raia ndio wanaowadhulumu{Majasusi na mahakimu}*

d. Ni mambo gani yaliyomtia Vuai machugachuga alipoachiliwa huru

i. *Hakuamini alikuwa kweli ameeachiliwa huru*

ii. *Alihofia kuamriwa asimame*

iii. *Alihofia kushikiwa bunduki*

e. Vuai anaelekea kuwa na Hulka gani?Fafanua kwa kurejelea kifungu

i. *Mwema –Anasema hajawahi kumponda mdudu*

ii. *Mwadilifu –Hataki kuyachafua mazingira*

iii. *Mkweli –Anacheza kwa uwazi sauti ya wayonge*

iv. *Msalihina-kupiga magoti na kuomba Mungu amwepushe na balaa nyingine*

f. Msamiati ufuatao una maana gani kwa mujibu wa kifungu

i. *Ombwe-kitu kilichowazi*

ii. *Mhemko-hamu kubwa ya kufurahia kitu*

## 2.UFUPISHO

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Kufufua na kuendeleza uchumi wa taifa ni jambo linalotegemea bidii na ambalo huchukua muda mrefu.Ili kufufua ba kuendeleza uchumi wan chi,mbinu zifuatazo zinafaa kuchukuliwa.

Kwanza ni bora kutegemeaa raslimali iliyomo nchini kwani suruali ya kuazima haisitiri matako.Ni lazima tukome kutegemea misaada  kutoka ng'ambo .Wahenga hawakuwa wendawazimu wwaliiposema kuwa mtegemea cha nduguye hufa maskini.

Bidhaa zinazonunuliwa kutoka ng'ambo hugharimu serikali kiasi kikubwa sana cha fedha.Tukiyatoshleza mahitaji yetu kwa kutumia bidhaa zinazotayarishwa nchini,uchumi wetu utaimarika.Raslimali ya nchi hutokan na ardhi yetu ina rtuba katika sehemu nyinngi.Tunamito,madini,maziwamisitu na madini mbalimbali kama vile dhahabu na aina zingine ammbazo hata hazijavumbuliwa bado.

Wakenya wengi hawaithmini kazi ya ukulima.Ukuzaji wa vyakula kwao ni kama kazi ya kijungu jiko ambayo huachiwa wasio na tengemeo linginemaishani.Mwelekeo huu ukibadilisha na tuwe na wakulima wathaminiao ukulima,uchhumi wa nchi utaboreshwa kwa kiwango kikubwa.Badala ya kukopa pesa nyingi aambazo huwa vigumu kulipa,nchi yetu inafaa iombe misaada.Jambo hili likitokea,wahisanni wetu katika nchi za kigeni wataelewa kwani sisi tumo katika taifa ambalo halijastawi kiuchumi.Jambo la kudai malipo kwa kutoza riba kubwa hudhoofisha mno hali ya uchumi wa mataifa yanayendelea.Riiba hutatiza mataifa yanayokopa jinsi kupe afanyavyo anapofyonza damu ya ndama bila huruma wala karaha.Kuwahimiza wananchi kujitegemea kwa kila njia ni jambo ambalo linaweza kuifaidi nchi yetu.Si lazima kila mtunaajiriwe ilia pate riziki.Sekta yajua kali ni mfano mzuri wa kuigwa ili wananchi wajitegemee.Hali hii itahakikisha serikali haitataabika ikijaribu kuwaajiri watu kazi ambazo hazipatikni kwa urahisi.

Hatua nyingine ni utulivu nchini .Nchi yoyote yenye rabsha miongni mwa wananchi wake haiwezi kupiga hatua mbele kiuchumi .Utulivu huwapa wananchi nafasi ya  kushughulikia wajibu wao wa ujenzi wa taifa. Michafuko ikiwepo,serikali hutumia pesa kununua zana za kivita kama vile bunduki za kutolea hewa ya machozi ili kukabiliana na sokomoko kila mara itokeapo.

Viongozi ni lazima wawe mfano bora katika harakati za kuuboresha uchumi.Mti ukifa shinale na tanzuze hukauka.Viongozi wenye nyadhifa mbalimbali nchini huwa si mfano mizuri.Wengi wao hujiingiza kwenye lindi la ufisadi ili kujinufaisha binafsi.Jambo hili

huwavunja mioyo kina yahe ambao hawana nafasi ya kufisidi wenzao.Uchumi wan chi hauwezi kuendeleza kwa njia hii.

Kazi za viwango vya juu kama vile uhandisi,urubani, unahodha na uanasheria nyakati nyingi hufanywa na wageni kutoka ng’ambo.Watu hawa hupata malipo ya hali ya juu sana.Ni bora serikali ibadili hali ili wenyeji wachukue nyadhifa hizi za kazi na kiasi cha mishahara kipunguzwe kidogo-na hapo nchi yetu itafaidika kiuchumi.Kwa kununua hisa za makampuni ya nje ,serikali itaundeleza uchumi kwa vile itakuwa na kibali cha kufaidika kutokana na faida zinazopatikana kwenye mkampuni hayo.

## Maswali

a. Eleza mambo yanayosaidia kuinua na kuendeleza uchumi

(maneno 60-70)(alama 7,1 utiririko))

*i. Kutegemea raslimali iliyo nchini*

*ii. Kutumia bidhaa zinazotayarishwa humu nchini*

*iii. Kuthamini kazi ya kilimo*

*iv. Nchi ziombe misaada badala ya mikopo*

*v. Watu wahimiziwe wajitegemee(wajiajiri)*

*vi. Kuwa na utulivu nchini*

*vii. Viogozi wawe mifano bora*

*viii. Wenyeji wapewe nyadhifa*

*ix. Serikali inunue hisa za nje*

*7*1=7*

b. Eleza mambo yanayokwamiza uchumi wan nchi

(maneno 60)(alama 6,1 utiririko))

*i. Kutegemea misaada kutoka nje*

*ii. Nchi kununua bidhaa kutoka ng’ambo*

*iii. Wakenya kutothamini kazi za ukulima*

*iv. Kukopa pesa nyingi  zenye riba ya juu*

*v. Kutengemea kazi ya kuajiriwa*

*vi. Kazi/nyadhifa za juu kupewa wageni*

*vii. Viongozi kutokuwa mifano bora*

*6*1=6*

3.MATUMIZI YA LUGHA

a. Huku ukizingatia jinsi hewa inavyozuiliwa,ainisha sauti zifuatazo;(alama 2)

(i)/y/…………kiyeyusho

(ii)/sh/……kikwamizo

(iii)/h/………kikwamizo

(iv)/ny/………nazali/kipua/king'ong'o

b. Andika neno lenye muundo ufuatao ;(alama 2)

i)irabu,irabu,irabu………………………aoa,aua aue

ii)irabu,konsonanti,konsonati,konsonati,irabu

……………………ombwe,imbwa,umbwa…………………

c. Ainisha mofimu katika maneno yafuatayo

(i)mwanao Mw-ngeli

an-mzizi

o- umiliki

(ii)azingatiaye

a-nafsi ya tatu umoja

zingati-mzizi

a-kauli

ye-kerejeshi

d. Onyesha aina za vielezi katika sentensi zifuatazo;(alama 2)

i)Barabara ndefu zaidi ilisakafiwa barabara

**zaidi-kielezi cha namna hali**

**barabara- kielezi cha namna halisi**

ii)Kiplagat alianza kula alipoambiwa asishike chakula hivi hivi

**kifisi- kielezi cha namna mfanano**

**hivi hivi- kielezi cha namna vikariri**

e. Andika sentensi ifuatayo kwa ukubwa;(alama 2)

Mwanamke huyu alibeba ndoo hizi hadi sokoni

**…Janajike hili lilibeba madoo haya hadi sokoni.**

f. Tunga sentensi yenye muundo ufuatao;(alama 2)

KN(RH+RH)+KT(t+V)

**Motto wa mama ni mrefu**

g. Tunga sentensi ukitumia neon alikuwa kama

i)Kitenzi kishirikishi kikamilifu;(alama 1)

**Mama <u>alikuwa</u> analala.**

ii) kitenzi kisaidizi;(alama 1)

**Mtoto <u>alikuwa</u> analala sebuleni.**

h. Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa;(alama 3)

Mwanasiasa alisema,”Mkinipigia kura nitawajengea zahanati kabla mwisho wa mwaka huu”

Mwanasiasa alisema kuwa iwapo wangempigia kura angewajengea zahanati kabla mwisho wa mwaka huo.

i. Nomino zifuatazo ziko katika ngeli gani;(alama 1)

i)ufizi……U-ZI

ii)firigisi…I-ZI

j. Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu

Waziri anasoma hotuba yake;(alama 1)

Waziri atakuwa amesoma hotuba.

k. Andika sentensi ifuatayo katika hali kanushi;(alama 1)

Nzige wengi walikuwa wanavamia maeneo hayo kabla ya serikali kuchukua hatua

Nzige wengi hawakuwa wanavamia maeneo hayo kabala serikali kuchukua hatua.

l. Bainisha kiima na yambwa katika sentensi ifuatayo;(alama 3)

Mama alimpikia mgeni wetu nyama ya kuku

Kiima-mama

Mgeni wetu-yambwa tendewa

Nyama ya kuku-Yambwa tendewa

m. Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo;(alama 2)

Mwalimu aliyetuzwa jana alifundisha shairi lililotungwa na Kezilahabi

Mwalimu aliyetuzwa jana-kishazi tegemezi

Alifundisha shairi lililotungwa na Kezilahabi -kishazi huru

Alifundisha shairi- kishazi huru

Lilotungwa na Kezilahabi-kishazi tegemezi

n. Tunga sentensi moja kutofuatisha maana ya **daka** na **taka**;(alama 2)

Daka-shika/kamata

Taka-uchafu,kusudia/penda

o. Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili ya kiambishi ka

Ka-amri km.Kaeni chini! Kamwambie aje.

Ka-kitendokitafanyika wakati ujao,km.Atakayesoma,watakaoshiriki.

Ka-wakati usiodhihirika ,km.Waziri kajiuzulu.

p. Chaganua sentensi ifutayo kwa njia ya mistari;(alama 4)

Genge la wezi lilituvamia

S-KN+KT

KN-N+KH/KV

N-Genge

KH-H+N/KV-V+N

H/V-La

N-wezi

KT-T

T-lilituvamia

q. Bainisha virai katika sentensi ifuatayo;(alama 3)

Pikipiki iliyonunuliwa jana iliharibika karibu na mto

RN-pikipiki iliyonunuliwa jana

RT-iliharibika karibu na mto

RH-karibu na mto

r. Eleza majukumu yas sentensi ifuatayo;(alama 1)

Nipe kalamu yangu mara moja

Amri

s. Andika sentensi ifuatayo upya kwa kubadilisha maneno yaliyopigiwa mstari katika kauli zilizo mabanoni;(alama 2)

Kazi hii imekuwa(tendea) ngumu sana lakini siwezi kufa(tendeshwa)moyo

Kazi hii *imeniwia* ngumu sana lakini siwezi *kufishwa* moyo.

t. Taja methali inayoafiki maelezo yafuatayo;(alama 1)

Mtu anayetegemewa katika jamii akiondoka wanaomtegemea huwa mashakani

*Mti mkuu ukigwa wana wa ndege huyumba.*

4.ISIMU JAMII(ALAMA 10)

"Mwenye sikio amesikia.Usiwe kama mimi .Wapurukushe wote wakupotoshao.Fuata ruwaza ya wanaokujali .Kwangu nimejishika sikio baada ya laity nyingi .Macho yamefumbuka.Usiseme nitazeekea huku.Lengo langu ni kuwahi uzamili na hata uzamifu.Kwani kuitwa profesa ni kosa?Niwafae wengine kimasomaso na kihali"

a. Taja na kuthibitisha sajili ya mazugumzo haya

*Sajili ya mawaidha/ushauri/wosia/nasaha.*

*Mzungumzaji anamtolea msikilizaji nasaha asifuate mkondo mbaya wa maisha aliyofuata*

b. Tambua mazigira ambamo mazungumzo haya yanatokea

*Shuleni/chuoni/taasisi ya elimu-anaiotoa nasaha hii kwa wenzake akiwa chuoni kwa sababu anasemawasidhani atazeeka huko,lengo ni kupata shahada*

c. Eleza sifa zozote saba za lugha zilizotumika kwenya mazungumzo haya

*a. Lugha iliyojaa matumini-anawania kupata uzamifu*

*b. Utohozi-profesa-professor*

*c. Swali balagha-kwani kuitwa professor ni kosa*

*d. Lugha ya kuonya-mwenye sikio amesikia*

*e. Nahau-nimejishika sikio-nimejirekebisha*

*f. Lugha sanifu-Kifungu kizima kimetumia lugha ipasavyo*

*g. Lugha ya maelezo-wapurukushe wote wakupotoshao fuata ruwaza ya wanaokujali*

*h. Msemi –macho yamefumbika-amezinduka*

*i. Matumizi ya msamiati wa taaluma ya kiusomi-uzamifu na profesa*

j. Matumizi ya sentensi fupi fupi-Usiwe kama mimi

*k. Lugha inayotumia taswira-anapotolea nasaha anasema usiwe kama mimi picha ya pengine jinsi alivyothurika inajitokeza akilini*

*l. Lugha imejaa hekima –anasema fuata ruwaza ya wanaokujali(ushauri anatoa unaongozwa na busara kwa Yule hataki msikilizaji ahasirike)*